Kuwasaidia wazee kuepuka *unyanyasaji wa kifedha*



Nini maana ya Unyanyasaji wa kifedha?

Sisi tunajua kuwa watu wa zaidi ya umri wa miaka 50 wako kwenye hatari ya kunyanyaswa kifedha, kashfa na udanganyifu. Hii inaitwa unyanyasaji wa wazee kifedha. Unyanyasaji wa kifedha unajumuisha wa matumizi ya fedha haramu au yasiyofaa au mali ya mtu na mtu mwingine ambaye ana uhusiano naye. Njia hii ya unyanyasaji inaweza kuchukua aina nyingi na kutokea kwa mtu yeyote, mara nyingi huanzia kidogo sana kuliko unavyofikiria.

Aina za kawaida za unyanyasaji wa kifedha kwa mzee

Unyanyasaji wa wazee unaweza kuchukua njia nyingi na inaweza kujumuisha vitendo vya kurudiwa au mara moja, vitisho au hata ukosefu wa kuchukua hatua. Hapa kuna aina kadhaa za kawaida za unyanyasaji:

Matumizi mabaya ya nguvu ya wakili

Hii inaweza kutokea wakati mtu mwenye idhini (wakili wako) anachukua pesa yako au mali kwa ajiri yake mwenyewe.

Shinikizo, vitisho na kutishiwa.

Hii ni wakati mtu anajaribu na kukulazimisha kusaini juu ya mali zako au anadai kwa lazima kuwa katika miradhi yako.

Udanganyifu na kashfa

Hizi hufanyika wakati mtu kwa makusudi anajaribu kupata imani yako ili kuiba pesa zako.

Kunyanyasa makubaliano ya familiaa

Hapa ndipo mikataba yoyote isiyo rasmi uliyonayo na familia juu ya pesa au mali inavunjwa au kuchukuliwa kama faida.

Matumizi mabaya ya fedha

Hii ni wakati mtu ambaye umemuruhusiwa kufikia pesa zako kuweza kuzitumia tofauti na jinsi ilivyokubaliwa

Mshtuko wa kihemko

Hii ni wakati mtu anatishia ili apate faida ya kifedha - kama vile kukataa kupewa wajukuu isipokuwa mkopo umetolewa.

Urithi wa kimyakimya

Hii ni wakati watu wazima, mara nyingi wanachama wa familia, hujihisi kuwa na haki ya pesa yako na mali na inaweza kusababisha kujaribu na kuzichukua kutoka kwako.

Mdhamini kufanya makosa

Wakati mwingine, licha ya kuwa hakuna nia mbaya, dhamana ya mkopo inaweza kwenda vibaya na kusababisha kupoteza nyumba yako au mali zingine.

Kushidwa kutoa malezi yaliyoahidiwa

Hii ni wakati mpangilio wa ndugu wa familia wa kutoa malezi unapovunjika.

Commonwealth Bank of Australia ABN 48 123 123 124 AFSL and Australian credit licence 234945.

Nani yuko hatarini?

Wakati unyanyasaji mkubwa wa kifedha unaweza kutokea kwa kila mtu, kuna vikundi fulani ambavyo viko kwenye hatari kubwa. Hii inajumuisha :

- Watu ambao wako peke yao au wametengwa
- Watu wenye ulemavu wa mwili au kiakili
- Watu wenye uelewa mdogo wa pesa kutokana na upungufu wa lugha au matatizo ya kiutamaduni
- Watu kutoka jamii za LQBTIQ +
- Watu ambao wanategemea wengine kwa malezi yao
- Watu ambao wamekuwa chini ya aina nyingine za dhuluma hapo zamani.

Kutambua unyanyasaji wa kifedha

Licha ya kuongezeka kwa udhalilishaji, unyanyasaji wa mzee wa kifedha unaweza kuwa mugumu kutambua na kuelewa kwa sababu mara nyingi hufichwa au kupunguzwa.

Kwa sababu hizi, ni kawaida kwa watu kuhisi aibu, migongano pamoja na kuzidiwa wakati wa kuzungumza juu ya unyanyasaji wa kifedha. Mara nyingi ni ngumu kwa watu wanaokabiliwa na unyanyasaji wa kifedha kuijua na kuidhibiti pamoja na/au kuitambua kwao pamoja na kwa watu wengine.



Ishara za onyo za kuzingatia:

1. Kuna uondoaji wa pesa ambao hauleti maana
2. Vizuizi vya lugha hufanya iwe ngumu kwako kuelewa
3. Unakosa au unachanganya taarifa za benki
4. Unahisi urafiki au kudhibitiwa na mtu na unaamini lazima ufanye kile mtu anachosema
5. Mtu ambaye hana mamlaka juu ya pesa zako kuongozana na wewe kwenda benki kutoa pesa
6. Mtu mwingine kujaza fomu za benki kwa niaba yako

Mzee kunyanyaswa kwa simu

Ikiwa wewe una wasiwasi wowote tafadhali piga simu 1800 ELDERHelp (1800 353 374).

Hii ni nambari ya simu ya bure ambayo hutoa habari pamoja na Ushauri juu ya unyanyasaji. Utaelekezwa moja kwa moja kwa huduma ya laini ya simu iliyopo ndani ya eneo lako. Mstari wa simu umeanzishwa kwa kushirikiana na serikali za jimbo na wilaya.

Unyanyasasaji wa Wazee kwa njia ya simu siyo huduma za msaada wa shida, na masaa ya kufanya kazi na huduma hutofautiana maeneo yote.

Ikiwa una wasiwasi wowote juu ya fedha zako tafadhali julisha benki yako.
Meneja wako wa mahali anaweza nasema nawe kibinafsi ikiwa unapenda hivyo.

Kwa maelezo zaidi kuhusu unyanyasaji wa mzee wa kifedha & utapeli unaweza kupakua mwongozo salama kwenye Tovuti ya CommBank.

Kumbuka: Hati hii inapatikana katika lugha zingine.